



89 Petro na Yohana wanaponya mtu kiwete

Kwa Biblia

Matendo ya Mitume mlango wa 3 na mlango wa 4:1 – 21

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Yesu alikuwa bado anasaidia wanafunzi wake hata baada ya kuenda Mbinguni

Somo

Siku moja wakati wa jioni, Petro na Yohana walienda kusali Hekaluni. Walipitia katika Mlango Mzuri wakiingia kwa Hekalu. Kulikuwa na kiwete aliyekaa kwa Mlango Mzuri. Huyu mtu alikuwa amekuwa kiwete maisha yake yote.
Hangeweza kutembea. Hangeweza kufanya kazi. Hakuwa na pesa. Kila siku huyu mtu alibebwa na kuwekwa kwa Mlango Mzuri. Aliomba pesa ili aende anunue chakula.



Petro na Yohana walifika kwa Mlango Mzuri. Huyo kiwete aliwaomba pesa. Petro na Yohana walisimama alikokuwa kiwete.

Maswali

1. Mbona Petro na Yohana walienda Hekaluni?
2. Waliona nani kwa Mlango Mzuri?
3. Kiwete aliuliza Petro na Yohana nini?
4. Petro alimfanya nini kiwete?
5. Petro aliambia umati nini?
6. Wakuu wa Hekalu walifanya nini?
7. Petro aliponya kiwete kwa jina la nani?
8. Wakuu wa Hekalu waliamrisha Petro na Yohana eti nini?
9. Petro na Yohana walijibu eti nini?
10. Wakristo wangapi walikuwa Yerusalemu wakati wa huo muujiza?

Majibu

1. Petro na Yohana walienda Hekaluni kusali.
2. Waliona mtu kiwete kwa Mlango Mzuri akiomba.
3. Huyo kiwete aliuliza Petro na Yohana wampee pesa.
4. Petro alimponya huyo kiwete. Sasa angetembea na kuruka.
5. Kwamba Mungu alikuwa amemfufua Yesu kutoka kwa wafu. Yesu aliwapa uwezo kutoka kwa Mungu kuponya mtu kiwete.
6. Wakuu wa Hekalu waliweka Petro na Yohana gerezani.
7. Walikuwa wamemponya katika jina la Yesu, mwenye wakuu walislubisha na Mungu akamfufua.
8. Waliwaamru kwamba wasizungumze wala kufundisha juu ya Yesu.
9. "Mungu alituamru tufundishe juu ya Yesu. Ni haki sisi kutii nyinyi badala ya Mungu?"
10. Wakriso kama elfu tano walikuwa Yerusalemu.

Petro na Yohana walimkazia huyo kiwete macho. Petro alimwambia, "Tuangalie sisi." Kiwete akafikiri wanataka kumpa pesa. Petro alimwambia tena, "Sina pesa zozote. Nitakupa nilichonacho. Katika jina la Yesu kristo simama na utembee."

Petro alishika mkono wa yule kiwete. Alimsaidia kusimama. Bunde tu, miguu yake ikapata nguvu. Alikuwa ameponywa! Huyo kiwete alitembea na kuruka na kumsifu Mungu. Aliingia kwa Hekalu pamoja na Petro na Yohana. Alikuwa anatembea na kuruka na kusifu Mungu.



Watu wote walimtambua huyo kiwete. Walikuwa wakimwona kwa Mlango Mzuri akiomba. Walishangaa kuona kwamba Petro na Yohana walikuwa wameponya. Umati wa watu ulikusanya kwa wakimwona akitembea na kuruka. Petro alizungumzia umati.

Petro aliwambia kwamba nguvu za Mungu ndizo zilimponya huyo kiwete. Petro aliambia watu habari njema. Mungu alikuwa amemfufua mwanawe Yesu kutoka kwa wafu. Yesu aliwapa uwezo kutoka kwa Mungu kumponya mtu huyu kiwete. Watu wengi waliamini na wakabatizwa. Kulikuwa na Wakristo Yerusalem kama elfu tano .

Wakuu wa Hekalu waliona vibaya kwa sababu watu wengi walikuwa na imani kwa Yesu. Petro alipokuwa bado anazungumza na watu, wakuu wa Hekalu walikuja. Walishika Petro na Yohana kwa sababu walikuwa wanasema kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu. Hao wakuu waliweka Petro na Yohana gerezani.

Kesho yake asubuhi, Petro na Yohana walipelekwa na wakuu wa Hekalu mbele ya hakimu. Hao wakuu waliuliza Petro na Yohana, "Ni kwa uwezo wa nani mliweza kufanya huu muujiza wa kuponya huyu kiwete?" Mungu alisaidia Petro na Yohana kuwajibu kwa hekima. Walisema, "Tuliponya huyu kiwete kwa jina la Yesu Kristo. Mlisulubisha Yesu. Mungu amemfufua kutoka kwa wafu. Huyu mtu kiwete aliponywa katika jina la Yesu."

Wakuu wa Hekalu walishangaa kuona kwamba Petro na Yohana walikuwa wameponya kiwete. Hawa wakuu hawangeweza kusema lolote kinyume kwa muujiza huu kwa sababu yule mtu aliyeponywa alikuwa amesimama nao pale.

Wale wakuu wa Hekalu waliwaamrisha Petro na Yohana kwamba, "Msizingumze wala kufundisha juu ya Yesu tena." Petro na Yohana walijibu, "Mungu ametwaamrisha tufundishe juu ya ufufuo wa Yesu. Ni haki sisi kutii nyinyi badala ya Mungu? Hatuwezi kuacha kufundisha juu ya Yesu."

Hakimu aliamrisha tena Petro na Yohana wasifundishe juu ya Yesu. Halafu wakawaachilia waende. Kila mtu alisifu Mungu kwa sababu Petro na Yohana waliponya mtu kiwete. Wakuu hawangeweza kuwaadhibu kwa sababu ya kufanya huo muujiza.

Petro na Yohana walienda kwa wanafunzi. Waliwambia kila kitu chenye wakuu wa Hekalu walisema. Wanafunzi wote walimtukuzza na kumsifu Mungu. Mungu alikuwa amewabariki. Petro na Yohana walikuwa huru tena. Watu wengi waliamini Mungu kwa sababu waliona mtu aliyejikuwa kiwete ameponywa.